# 8. Viua wadudu ghushi na visivyo halali

## Mada ya 8a

## Bidhaa ghushi na zisizo halali ni zipi?

# JARIDA LA UHAKIKA

## 8. Viua wadudu ghushi na visivyo halali

## <u>Mada ya 8a:</u> Bidhaa ghushi na zisizo halali ni zipi?

Majina mengi tofauti yanaweza kutumiwa kuelezea bidhaa ghushi na zisizo halali kama vile bandia, buni, haramu na iga. Katika kitabu hiki cha mwongozo wa mafunzo, tutatumia majina "ghushi" na "zisozo halali" ili kuelezea bidhaa hizi.

**Bidhaa ghushi na zisizo halali ni zipi?**
Sheria imepiga marufuku kuuza au kununua bidhaa ghushi na zile zisizo halali. Kwa hali zote mbili, hakuna usaidizi kwa mnunuzi baada ya mauzo ya bidhaa hii.

Kuna tofauti kati ya ghushi na zisizo halali.

**Ghushi**
Bidhaa ni ghushi kama **sio halisi** (sio ya asili/ya kwanza). Hii yaweza kuonekana kwa njia mbali mbali:

- **Nakala** inayofanana sana na bidhaa halisi. Katika hali hii bidhaa inaweza kuwa na ubora wa juu lakini haijatengenezwa na mtengenezaji halisi/wa kwanza na basi ni ghushi.
- **Kilichomo ndani** (Kiambato kitendaji) kinatofautiana na kile kinachodaiwa ndicho.
- Viambato ni vya **hali duni**.
- **Kibandiko cha maelezo** ni tofauti na kile kilicho halisi. Mara nyingi bidhaa ni bora lakini tarehe ya mwisho wa matumizi imepita.
- **Kifurushi au pakiti** ni tofauti. Hii inawezekana kama bidhaa halisi ilibadilishwa na kuwekwa katika pakiti tofauti.

**Zisizo halali**
Bidhaa sio halali kama **haijasajiliwa** nchini ambamo inauzwa. Kuna uwezekano wa kuwa bidhaa ni bora na inauzwa katika nchi jirani lakini haijaidhinishwa nchini ambapo inauzwa, au bidhaa iko katika njia ya kusajiliwa.

**Bidhaa halisi na halali zikilinganishwa na bidhaa ghushi na zisizo halali**

| | Halisi na Halali | Ghushi na zisizo halali |
|---|---|---|
| **Kazi ya utafiti na ustawi** | Ilitekelezwa | Haikutekelezwa |
| **Kibandiko cha** | Kina maagizo na mapendekezo | Maagizo na mapendekezo |

| | | |
|---|---|---|
| **maelezo** | ya kutegemewa | kwenye kibandiko cha maelezo hayawezi kuaminika |
| **Kuidhinishwa na utawala wa mitaani** | Ndio | Hapana |
| **Huduma kwa wateja** | Kama kuna kasoro na bidhaa, unaweza kulalamika kwa mtengenezaji | Mtengenezaji hatambulikani, kwa hivyo huwezi kulalamika kama kuna kasoro |
| **Viambato vitendaji** | Kilichomo ndani, muundo na viambato vitendaji vinalingana na maandishi kwenye kibandiko cha maelezo | Kilichomo ndani, muundo na viambato vitendaji havina uhakikisho |

**Kwa nini ipo tofauti ya bei kati ya bidhaa halisi na ghushi?**

Watengezaji wa bidhaa halisi hutumia pesa nyingi sana kwa ustawi, uchanganuzi, majaribio, kudhibiti ubora na usajili wa bidhaa kabla ya kuingizwa sokoni. Watengenezaji wa bidhaa ghushi na zisizo halali hawana gharama hizi. Wanatumia njia za mkato kuleta bidhaa zao kwenye soko.

# MAELEZO YA ZIADA

## 8. Viua wadudu ghushi na visivyo halali

**<u>Mada ya 8a:</u>** Bidhaa ghushi na zisizo halali ni zipi?

**Kwa nini kuna mbolea ghushi?**
Katika miaka mingi iliopita, bei ya mbolea imeongezeka sana jambo ambalo limefanya wakulima maskini washindwe kununua mbolea. Pia hawawezi kupata mkopo wa kununua mbolea. Wanabiashara walaghai na wasio halali waligundua kwamba kuna haja ya mbolea ya bei nafuu. Walitumia hali hii ili kuagiza mbolea ghushi na bandia hadi nchini kutoka nchi za ng'ambo.

**Ni ipi mikakati ya soko ya biashara ya mbolea isio halali?**
Waduhuli na wauza bidhaa hulenga wakulima maskini katika sehemu za mashambani au za mbali. Wakulima hawa hununua viwango vidogo bila kuandikishana. Wauza bidhaa hawa huja katika sehemu hizi na bidhaa zao, hukusanya pesa na kupotea hadi msimu ujao ambapo watajitokeza tena katika sehemu nyingine ya mashambani/ya mbali.

# MWONGOZO

## 8. Viua wadudu ghushi na visivyo halali

## <u>Mada ya 8a:</u> Bidhaa ghushi na zisizo halali ni zipi?

### Vifaa vinavyohitajika:

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi
- ☑ Karatasi kubwa

### Muda unaohitajika: Dakiki 45

### Maandalizi:

- ☑ Karatasi ilio na kichwa: *Bidhaa ghushi na zisizo halali ni zipi?*
- ☑ Seti tatu za kadi za rangi zilizo na maandishi yaf:
  - Ilitekelezwa
  - Haikutekelezwa
  - Hutegemewa
  - Haiaminiki
  - Ndio
  - Hapana
  - Uwezekano wa malalamishi
  - Mtengenezaji hatambuliki
  - Inalingana na kibandiko cha maelezo
  - Haijahakikishwa
- ☑ Majedwali matatu kwenye karatasi kubwa yaliyo na yafuatayo:

| | Halisi na Halali | Ghushi na zisizo halali |
|---|---|---|
| **Kazi ya utafiti na ustawi** | | |
| **Kibandiko cha maelezo** | | |
| **Kuidhinishwa na utawala wa mitaani** | | |
| **Huduma kwa wateja** | | |

| Viambato vitendaji | | |
|---|---|---|

# Mwanzo

| | |
|---|---|
| **U**sikivu: | Waambie washiriki kwamba, wiki iliyopita ulinunua kwa bei rahisi saa ya mkononi ya rolex kwa dola kumi kutoka kwa muuzaji. Uliza washiriki wanachofikiria kuhusu saa yako ya bei nafuu. Watakwambia kwamba ulinunua saa bandia. Kataa na uwambie kwamba ni halisi. Hawatakubaliana nawe. Waulize ni kwa nini? Wacha wakuridhishe kwamba ulinunua rolex bandia. Waambie kwamba bidhaa ghushi na visivyo halali hupatikana katika kila sekta ikiwemo sekta ya kilimo. Katika kila soko tutapata bidhaa ghushi na zisizo halali. |
| **K**ichwa: | Ambia washiriki kichwa huku ukiwaonyesha karatasi iliyo na kichwa/maandishi: *Bidhaa ghushi na zisizo halali ni zipi?* |
| **K**usadikika: | Elezea uzoefu wako katika pembejeo za kilimo |
| **M**alengo: | Kuelezea bidhaa ghushi na zisizo halali ni zipi na tofauti baina ya bidhaa halisi na bidhaa ghushi au zisizo halali. |
| **M**anufaa: | Ukijua bidhaa ghushi na zisizo halali ni gani,utaweza kuepuka dhidi ya biashara isio halali. |
| **M**welekeo: | Katika kipindi hiki, tutaangazia ufafanuzi wa bidhaa ghushi na zisizo halali. Hatutajadili matokeo yake. |

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waambie washiriki kwamba kwenye kichwa tumetumia bidhaa **ghushi na zisizo halali.** Uliza kama yeyote anaweza kutaja majina mbadala ya bidhaa ghushi na zisizo halali. Labda watasema bandia au buni. Waambie kwamba katika mafunzo haya tutatumia ghushi na zisizo halali.
2. Waambie washiriki kwamba ni kinyume cha sheria kununua au kuuza bidhaa ghushi na zisizo halali. Ongezea kwamba kuna **tofauti** kati ya bidhaa ghushi na zisizo halali.
3. Uliza kama yeyote anaweza kueleza maana ya bidhaa **ghushi.** Bidhaa ni ghushi kama **sio halisi** (sio za asili/kwanza). Uliza kama yeyote anaweza kutoa mfano wa vile bidhaa ghushi zinaweza kutambuliwa. Pokea majibu kadhaa na uhakikishe yafuatayo yametajwa:
   - **Nakala** inayofanana sana na bidhaa halisi. Katika hali hii bidhaa inaweza kuwa na ubora wa juu lakini haijatengenezwa na mtengenezaji halisi/wa kwanza na basi ni ghushi.

- **Kilichomo ndani** (Kiambato kitendaji) kinatofautiana na kile kinachodaiwa ndicho.
- Viambato ni vya **hali duni**.
- **Kibandiko cha maelezo** ni tofauti na kile kilicho halisi. Mara nyingi bidhaa ni bora lakini tarehe ya mwisho wa matumizi imepita.
- **Kifurushi au pakiti** ni tofauti. Hii inawezekana kama bidhaa halisi ilibadilishwa na kuwekwa katika pakiti tofauti.

4. Uliza kama yeyote anaweza kueleza maana ya bidhaa **zisizo halali**:

   Bidhaa sio halali kama **haijasajiliwa** nchini ambamo inauzwa. Kuna uwezekano kwamba bidhaa ni bora na inauzwa katika nchi jirani lakini haijaidhinishwa nchini ambamo inauzwa au iko katika njia ya kusajiliwa.

5. Gawanya washiriki katika vikundi vitatu. Patia kila kikundi jedwali tupu, na kundi la kadi za rangi zilizo na maandishi ya maelezo juu ya bidhaa halisi, ghushi na zisizo halali. Waambie washiriki waweke kadi hizo mahali palipo sahihi kwenye jedwali. Kadi moja kwa kila tundu. Wape muda wa kutosha kubandika kadi zote katika jedwali.
6. Kila kikundi kibandike jedwali lililokamilishwa ukutani halafu vijadili tundu baada ya tundu. Ona kama vikundi vinakubaliana na kama havikubaliani, jadili mahali kadi hiyo inafaa kuwa. Matokeo ya mwisho ni:

| | **Halisi na Halali** | **Ghushi na zisizo halali** |
|---|---|---|
| **Kazi ya utafiti na ustawi** | Ilitekelezwa | Haikutekelezwa |
| **Kibandiko cha maelezo** | Kina maagizo na mapendekezo ya kutegemewa | Maagizo na mapendekezo kwenye kibandiko cha maelezo hayawezi kuaminika |
| **Kuidhinishwa na utawala wa mitaani** | Ndio | Hapana |
| **Huduma kwa wateja** | Kama kuna kasoro na bidhaa, unaweza kulalamika kwa mtengenezaji | Mtengenezaji hatambulikani, kwa hivyo huwezi kulalamika kama kuna kasoro |
| **Viambato vitendaji** | Kilichomo ndani, muundo na viambato vitendaji vinalingana na maandishi kwenye kibandiko cha maelezo | Kilichomo ndani, muundo na viambato vitendaji havina uhakikisho |

# Malizia

Muhtasari: Patiana ufafanuzi wa bidhaa ghushi na zisizo halali. Taja tofauti kati ya bidhaa halisi ni zile ghushi na zisizo halali.

Maswali Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Uliza bidhaa ghushi ni zipi. Uliza bidhaa zisizo halali ni zipi. Uliza baadhi ya tofauti kati ya bidhaa halisi na bidhaa ghushi na zisizo halali.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki tumejifunza kuhusu bidhaa ghushi na zisizo halali. Katika vipindi vingine tutajadili matokeo ya matumizi ya bidhaa hizi na vile tunaweza kuzitambua

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.